MAAZIMIO YA MKUTANO WA WADAU WA SEKTA YA MIFUGO ULIOFANYIKA DODOMA
TAREHE 28-30 SEPTEMBA 2009

NA.	HOJA	AZIMIO	MUDA WA UTEKELEZAJI	MHUSIKA
1.	Upatikanaji wa Ardhi, Maji na Malisho kwa ajili ya Mifugo	(i) Serikali isimamie utekelezaji wa "National Land use Masterplan" ili kukamilisha utengaji, upimaji, umilikishaji maeneo ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.	Mwaka 1- 5 kuanzia 2010/2011	Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi
		(ii) Maeneo ya ardhi yaliyopimwa na kumilikishwa ambayo hayatumiki katika uzalishaji yarudishwe Serikalini na Serikali iwagawie wawekezaji wengine.	2009/2010	Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi
		(iii) Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na sekta binafsi ziwekeze katika miundombinu ya maji (malambo, mabwawa na visima) kwa ajili ya mifugo.	Mwaka 1- 5 kuanzia 2010/2011	Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekta Binafsi
		(iv) Mashamba ya kuzalisha mbegu bora za malisho yaimarishwe na kuanzisha mengine pamoja na teknolojia ya utunzaji wa malisho wakati wa kiangazi.	Mwaka 1- 5 kuanzia 2010/2011	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekta Binafsi
		(v) Wafugaji wahimizwe kuendeleza na kuhifadhi malisho katika maeneo yao kwa ajili ya matumizi ya kiangazi.	Muda wote	Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekta Binafsi
2.	Uendelezaji wa Miundombinu katika Sekta ya Mifugo	(i) Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi ziongeze uwekezaji katika kujenga na kuimarisha miundombinu ya mifugo ikiwemo majosho, malambo, minada, vituo vya afya ya mifugo, vituo vya ukaguzi wa mifugo, machinjio na njia za mifugo.	2010/2011 na kuendelea	OWM – TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na Sekta binafsi

NA.	HOJA	AZIMIO	MUDA WA UTEKELEZAJI	MHUSIKA
		(ii) Mamlaka za Serikali za Mitaa na Serikali za vijiji zitunge na kusimamia sheria ndogo za matumizi endelevu ya miundombinu ya mifugo.	2010/2011 na kuendelea	OWM – TAMISEMI na Mamlaka za Serikali za Mitaa
3.	Uwekezaji na Vivutio vya Uwekezaji katika Sekta ya Mifugo	(i) Serikali iondoe kodi na vikwazo mbalimbali vinavyokwamisha uwekezaji.	2009/2010	Wizara ya Fedha na Uchumi
		(ii) Serikali iongeze bajeti kwa sekta ya mifugo ili kuwezesha kuibua miradi mikubwa katika Mamlaka ya Serikali ya Mitaa.	2010/2011	Wizara ya Fedha na Uchumi, Mamlaka za Serikali ya Mitaa
		(iii) Serikali iwezeshe Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) na sekta binafsi kununua ng'ombe kutoka kwa wafugaji na kuwanenepesha pamoja na kuingia katika uzalishaji wa mkataba (contract farming).	Kuanzia 2010/2011	Wizara ya Fedha na Uchumi, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) na Sekta binafsi
		(iv) Serikali iharakishe uanzishwaji wa benki ya kilimo.	2009/2010	Wizara ya Fedha na Uchumi
		(v) Serikali iwezeshe mabenki mbalimbali kufungua madirisha yatakayotoa mitaji ya uwekezaji kwenye mifugo kwa kuanzia na TIB na kuongeza mtaji kwenye Mfuko wa Pembejeo.	2010/2011	Wizara ya Fedha na Uchumi, Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika
		(vi) Mamlaka za Serikali za Mitaa zitekeleze agizo la kutenga asilimia 15 ya mapato yatokanayo na mifugo na mazao yake kwa ajili ya kuendeleza Sekta ya Mifugo.	2009/2010 na kuendelea	Mamlaka za Serikali za Mitaa
4.	Aina ya Mifugo	(i) Serikali iimarishe mashamba ya kuzalisha mifugo (LMUs) bora yaliyopo na ranchi za NARCO na kuanzisha mashamba mengine mapya 5 katika	2010/2011	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, mikoa ya Lindi, Rukwa,

NA.	HOJA	AZIMIO	MUDA WA UTEKELEZAJI	MHUSIKA
		mikoa ya Lindi, Rukwa, Kigoma, Tabora na Manyara kwa kushirikiana na sekta binafsi.		Kigoma, Tabora na Manyara na Sekta binafsi
		(ii) Sheria ya Uzalishaji Mbari Bora ya Wanyama (Animal Breeding Act) ikamilishwe.	2010/2011	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi
		(iii) Kituo cha Taifa cha Uzalishaji Mbegu Bora za Mifugo cha NAIC Usa River na vituo vya kanda vya uhimilishaji vilivyopo viimarishwe na kujenga vipya na wafugaji wahimizwe kutumia huduma za uhimilishaji.	2010/2011	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, OWM – TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekta binafsi
		(iv) Wizara iimarishe hifadhi ya vinasaba vya mifugo ya asili katika vituo vya Mpwapwa, Mabuki, Uyole, Naliendele na West Kilimanjaro na kuanzisha utunzaji mbegu za asili kwa njia ya kugandisha.	2010/2011	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na Taasisi za utafiti
5. 5.1	Viwanda na Masoko Kuongeza Thamani kwa Mazao ya Mifugo na Kuongeza Soko la Ndani na Mazao ya Mifugo	(i) Serikali iwezeshe NARCO na NDC na sekta binafsi kujenga na kuendesha viwanda vya kusindika nyama katika maeneo ya ufugaji yakiwemo ya mipakani. Aidha, ujenzi wa viwanda vya nyama vya Mbeya na Shinyanga ukamilishwe. Vile vile, mifugo iuzwe minadani kwa kutumia mizani.	2010/2011 hadi 2014/2015	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Fedha na Uchumi, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, NDC, NARCO na Sekta binafsi

NA.	HOJA	AZIMIO	MUDA WA UTEKELEZAJI	MHUSIKA
		(ii) Serikali ifanye tathmini ya makampuni yaliyopewa viwanda vya usindikaji wa mazao ya mifugo vikiwemo vya nyama, maziwa, ngozi na vyakula vya mifugo, ili kama yameshindwa kuviendesha, hatua stahiki zichukuliwe	2010/2011	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Fedha na Uchumi (CHC), Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko
		(iii) Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi ihamasishe matumizi ya bidhaa za mifugo zinazozalishwa hapa nchini zenye ubora na viwango ili kusisimua soko la ndani la bidhaa hizi.	2009/2010 na kuendelea	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, TBS, TFDA, LAT, Bodi za mazao ya mifugo na Sekta binafsi
		(iv) Majukumu ya TFDA na Bodi za Mazao ya Mifugo yapitiwe ili kuondoa migongano iliyopo.	2009/2010	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, TFDA na Bodi za mazao ya mifugo
		(v) Serikali kwa kushirikiana na Sekta binafsi ipanue Mpango wa Unywaji wa Maziwa Shuleni ikianzia kwenye mikoa yenye mifugo mingi.	2010/2011	OWM - TAMISEMI, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko

NA.	HOJA	AZIMIO	MUDA WA UTEKELEZAJI	MHUSIKA
5.2	Kuimarisha Uzalishaji, Ukusanyaji na Usindikaji wa Maziwa	Serikali ihamasishe uanzishaji na uimarishaji wa vikundi na vyama vya ushirika vitakavyojenga na kuendesha vituo vya kukusanyia maziwa.	2009/2010 na kuendelea	OWM – TAMISEMI, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Bodi ya Maziwa na Sekta binafsi.
6. 6.1	Utafiti, Mafunzo na Huduma za Ugani Kuimarisha Utafiti	(i) Serikali iboreshe mazingira, maslahi na vitendea kazi kwa watafiti na kuimarisha taasisi za utafiti zitambulike kisheria.	2010/2011	Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi
6.2	Kuimarisha Mafunzo na Huduma za Ugani	(i) Serikali iimarishe vyuo vya mafunzo ya mifugo kwa kuvitambua kisheria na kuboresha mazingira, maslahi na vitendea kazi kwa wakufunzi wa vyuo hivyo. Aidha, vyuo vya mafunzo ya mifugo vya Madaba, Tengeru, Temeke, Morogoro, Buhuri, Mpwapwa na vyuo vya mafunzo ya ufugaji vya Kikulula na Mabuki vipanuliwe ili kuongeza idadi ya udahili wa wanafunzi kutoka 1,200 kwa sasa hadi 3,000 kwa mwaka.	2010/2011 hadi 2011/2012	Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Mawasiliano Sayansi na Teknolojia

NA.	HOJA	AZIMIO	MUDA WA UTEKELEZAJI	MHUSIKA
		(ii) Serikali iweke vivutio kwa watumishi wa ugani kwa kuwapa vitendea kazi, nyumba, usafiri, mafunzo rejea na ya muda mrefu na vianzia mshahara.	2010/2011	Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, OWM – TAMISEMI, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi
		(iii) Serikali ivunje cheo cha Afisa Maendeleo ya Kilimo na Mifugo wa Wilaya (DALDO) na kurejesha cheo cha Afisa Mifugo wa Wilaya na Afisa Kilimo wa Wilaya.	2009/2010	OWM – TAMISEMI
		(iv) Mamlaka za Serikali za Mitaa ziajiri watumishi wa mifugo kujaza ikama kulingana na mahitaji.	2010/2011	Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, OWM – TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa
		(v) Sekretariati za mikoa ziajiri watumishi wa mifugo kulingana na ikama ili kuimarisha usimamizi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.	2010/2011	Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na OWM – TAMISEMI
6.3	Elimu kwa Wafugaji, Wasindikaji na Wafanyabiashara wa Mifugo	Mamlaka za Serikali za Mitaa zitoe elimu kwa wananchi ili waweze kuibua miradi mingi ya mifugo chini ya DADPs ikiwa ni pamoja na ufugaji bora, ujasiriamali na usindikaji.	2009/2010 na kuendelea	Mamlaka za Serikali za Mitaa
7.	Udhibiti wa Magonjwa ya Mifugo	(i) Mamlaka za Serikali za Mitaa zizingatie Sheria ya Magonjwa ya Mifugo Na. 17 ya 2003 na Sheria ya Ustawi wa Wanyama Na. 19 ya 2008 na kanuni zake katika kusafirisha mifugo nchini.	2009/2010 na kuendelea	Mamlaka za Serikali za Mitaa

NA.	HOJA	AZIMIO	MUDA WA UTEKELEZAJI	MHUSIKA
		(ii) Serikali ianzishe maeneo huru kwa magonjwa ya mifugo (Disease Free Compartments & Zones)	2010/2011 na kuendelea	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekta binafsi
		(iii) Serikali iongeze Ugonjwa wa Miguu na Midomo (FMD), Sotoka ya mbuzi na kondoo (PPR) na Ugonjwa wa Mapele ngozi (Lumpy skin disease) kwenye orodha ya magonjwa ya milipuko inayoyadhibiti moja kwa moja kama ilivyo kwa Ugonjwa wa Homa ya mapafu.	2010/2011	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na Mamlaka za Serikali za Mitaa
		(iv) Mamlaka za Serikali za Mitaa na Serikali za Vijiji zitunge sheria ndogo za kuwataka wafugaji kuogesha mifugo ili kudhibiti magonjwa yaenezwayo na kupe. Aidha, zifuatilie kwa karibu usambazaji na matumizi ya pembejeo hasa kwa ngazi ya kijiji kwa kuzingatia sheria hizo.	2010/2011 na kuendelea	Mamlaka za Serikali za Mitaa
		(v) Maabara Kuu ya Mifugo Temeke na SUA ziimarishwe katika utoaji huduma ya utafiti, utambuzi na ufuatiliaji wa magonjwa ya wanyama.	2010/2011	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na SUA
8.	Kuandaa Mpango wa kuendeleza sekta ya mifugo	(i) Serikali kwa kushirikiana na wadau iandae mpango wa kuendeleza sekta ya mifugo.	2010/2011	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na wadau wa sekta
		(ii) Wizara iratibu mipango ya kisekta inayotekelezwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.	2009/2010 na kuendelea	OWM- TAMISEMI, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na

NA.	HOJA	AZIMIO	MUDA WA UTEKELEZAJI	MHUSIKA
				Sekretarieti za Mikoa
9.	Ukusanyaji wa taarifa na takwimu za sekta ya mifugo	(i) Serikali kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa ifanye sensa kamili ya mifugo.	2011/2012	Wizara ya Fedha na Uchumi, Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi
		(ii) Serikali kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa iimarishe mfumo wa upatikanaji wa takwimu na taarifa za sekta ya mifugo.	2009/2010	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekretarieti za Mikoa
10.	Uvamizi wa mifugo kutoka nchi jirani	(i) Kuimarisha ulinzi na usalama wa Taifa mipakani ikiwa ni pamoja na kuanzisha shughuli za ufugaji katika maeneo ya mipakani hususan mkoa wa Kagera.	2009/2010	Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa
		(ii) Serikali iharakishe kuandaa mapendekezo ya kutunga sheria ya utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo kuweza kubaini mifugo iliyopo nchini.	2009/2010	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Katiba na Sheria
11.	Ushirikishwaji wa Chama Tawala na vyama vingine vya siasa	Chama Tawala, vyama vingine vya siasa, Asasi za kijamii, kidini, mashirika yasiyo ya kiserikali vihamasishe utekelezaji wa mipango inayolenga kuleta mapinduzi katika sekta ya mifugo.	2009/2010 na kuendelea	Chama Tawala na vyama vingine vya siasa